

Ujumuishaji wa Jinsia na Uchanganuzi

(kutoka kwenye nyenzo ya shirika la USAID ya Guide to Gender Integration and Analysis)

Unaweza kuchaguamaswali kulingana na jinsi yanavyohusiana na mgogoro na miktadha ya shughuli za VE katika eneo lengwa la mradi wako.

+ MASWALI YA JUMLA

- Hali na majukumu tofauti ya wanawake na wanaume katika jamii, ulingo wa kisiasa, kazini na nyumbani (kwa mfano, majukumu katika kufanya maamuzi) yataathiri aje mradi unaopaswa kutekelezwa?
- Matokea yanayotarajiwa ya mradi yataathiri aje wanawake na wanaume kwa njia tofauti?

+ WAJIBU NA MAJUKUMU YA KIJINSIA

- Hali na majukumu tofauti ya wanawake na wanaume na/au mabadiliko yoyote au kubadilika kwa miktadha hii kunachangia katika mitindo ya malalamiko ambayo hutumiwa kushawishi watu kuanzisha mgogoro wenye vurugu?
- Wajibu tofauti wa wanawake na wanaume nyumbani huwafanya wawe katika hatari kubwa au kutokuwa katika hatari ya uwezekano wa kukumbwa na mgogoro wenye vurugu?
- Wanaume na wanawake wana majukumu gani katika kushawishi watu kuanzisha mgogoro wenye vurugu au katika usuluhishaji wa mgogoro?
- Tofauti za nafasi zinazoshikiliwa na wanaume na wanawake katika jamii zinachangia katika hali yao ya kushiriki katika nafasi za uongozi na kwenye shughuli za jamii katika viwango vya eneo na kitaifa?
- Majukumu ya wanawake na wanaume nyumbani yanachangia jinsi maamuzi yanavyofanywa?

+ KANUNI NA MATARAJIO YA KIJINSIA

- Matarajio ya tabia za wanawake na wanaume yanaathiri uwezekano wao wa kushawishika kushiriki katika mgogoro wenye vurugu?
- Matarajio ya majukumu na tabia za wanawake na wanaume yanachangia katika malalamiko ambayo wahusika wakuu wanaweza kutumia kushawishi watu kushiriki katika mgogoro wenye vurugu?
- Kanuni za kitamaduni kuhusu tabia "inayokubalika" ya wanawake na wanaume zinachangia/kuzuia maarifa yao na kushiriki kikamilifu katika shughuli za usuluhishaji wa mgogoro/kukuza amani?
- Tofauti zinazokisiwa katika maarifa, michakato ya kufanya maamuzi na tabia za wanawake na wanaume zinaathiri mawasiliano na kushiriki habari katika jamii?

+ UFIKIAJI WA NYENZO, MAELEZO NA MAMLAKA

- Wavulana/wanaume na wasichana/wanawake wana uwezo sawa wa kufikia fursa na nyenzo katika jamii, kama vile elimu, maji, umiliki wa mashamba, haki na fursa za kiuchumi? Hali hii inaathiri aje uwezekano wa wanaume na wanawake kushawishika kushiriki katika matendo ya vurugu?
- Wanaume na wanawake wanashikilia mamlaka katika nyanja gani? Nyanja tofauti za mamlaka wanayoshikilia zina athari gani katika usuluhishaji wa mgogoro kwa ufanisi? Wahusika wakuu ni akina nani?
- Wahusika wa mgogoro hutumia vurugu za kijinsia kama mbinu yao? Wanaume na wanawake hutekeleza majukumu gani (kama waathiriwa, wakosaji, n.k.)? Vurugu hizi husababisha athari gani kwa familia, jamii na kijamii?
- Hali ya kutokuwa na usawa wa kufikia mapato ya familia husababisha tofauti ambazo huchangia katika uwezekano wa kutokea kwa mgogoro wenye vurugu?
- Wanaume na wanawake hukumbana na vizuizi tofauti wanapotafuta usalama katika maeneo ya mashambani?
- Utofauti wa uwezo wa wanaume na wanawake kufikia nyenzo muhimu na haki za umiliki wa mashamba huathiri uwezo wao wa kukabiliana na athari mbaya za mgogoro wenye vurugu maishani mwao na katika jamii?

+ MATOKEO YANAYOTARAJIWA YA MRADI YATAATHIRI AJE WANAWAKE NA WANAUME KWA NJIA TOFAUTI?

- Hali na majukumu tofauti ya wanawake na wanaume katika jamii, ulingo wa kisiasa, kazini na nyumbani (kwa mfano, majukumu katika kufanya maamuzi) yataathiri aje mradi unaopendekezwa?
- Hatua ya kuhimiza hali ya wanaume kushiriki katika mradi itadunisha au kukuza uhuru na hali ya kuwezesha kwa wanawake?
- Miradi kama hii iliyotekelezwa awali iliathiri aje miktadha ya kijinsia nyumbani na katika jamii?
- Kwa miradi ya uwezesaji wa wanawake, kuongezeka kwa maarifa ya wanawake ya kufikia nyenzo kutazidisha hatari yao ya kukumbana na vurugu za kinyumbani? Hatua ya kushirikishwa kwa wanaume itasaidia kushughulikia hatari hii?
- Shughuli za uwezesaji wa wanawake zitaathiri miktadha ya mamlaka nyumbani na ukabidhi wa nyenzo? Matokeo mabaya yasiyotarajiwa yanaweza kutokea? Unawezaje kuyashughulikia?
- Shughuli za upatanisho na kuleta amani zinazopendekezwa zitashughulikia vizuizi vinavyohusiana na kanuni za kijinsia na kutokuwa na usawa?

Baada ya kuchagua maswali yako, tumia jedwali la kazi lililo hapa chini kuyajibu.

MASWALI YA JUMLA	
WAJIBU NA MAJUKUMU YA KIJINSIA	
KANUNI NA MATARAJIO YA KIJINSIA	
UFIKIAJI WA NYENZO, MAELEZO NA MAMLAKA	
MATOKEO YANAYOTARAJIWA YA MRADI YATAATHIRI AJE WANAWAKE NA WANAUME KWA NJIA TOFAUTI?	